*Nordic Journal of African Studies 11(2): 185-197 (2002)*

# Nafasi Ya Kiswahili Katika Ujenzi Wa Jamii Mpya Ya Afrika Mashariki

JOHN G. KIANGO
*University of Dar es Salaam, Tanzania*

## UTANGULIZI

Lugha ni chombo muhimu sana cha mawasiliano kilichoundwa na sauti za nasibu za kusemwa na kutumiwa na jamii ya utamaduni fulani. Jinsi ambavyo zipo jamii nyingi za tamaduni mbalimbali duniani, vivyo hivyo ziko lugha mbalimbali zilizoundwa kukidhi haja ya mawasiliano ya tamaduni mbalimbali.

Maingiliano ya jamii zenye tamaduni na lugha mbalimbali yanayotokana na mashirikiano katika shughuli za biashara na nyinginezo za kijamii, huzusha haja ya kuwepo kwa lugha moja itakayoweza kuwaungaanisha watu hao wenye tamaduni na lugha mbalimbali. Maingiliano kama hayo yanaweza kuwa katika viwango mbalimbali. Kiwango cha kwanza ni kile cha mtu binafsi ambapo mtu hutoka kwenye jamii yake na kwenda kuishi kwenye jamii inayozungumza lugha tofauti na ile ya kwao. Katika hali kama hiyo, mtu huyo itabidi ajifunze lugha ya jamii ile ya pili ili aweze kuwasiliana nao. Kiwango cha pili ni kile kinachohusisha mkusanyiko wa watu waliotoka kwenye tamaduni mbalimbali na hawana hata lugha moja ya kuwaunganisha. Watu kama hawa wakikaa pamoja huweza kuzusha lugha ya kati ambayo katika hatua za mwanzo itajulikanazo kama pijini na baadaye kama krioli. Kiwango cha tatu ni kile ambacho maingiliano ya watu wenye tamaduni na lugha mbalimbali husababisha kuteuliwa kwa lugha moja miongoni mwa lugha zao na kutumika kama chombo cha mawasiliano na cha kuziunganisha jamii zote husika. Kiwango hiki chaweza kujitokeza katika ngazi ya wilaya, mkoa, nchi, kanda, bara na hata ulimwengu mzima.

Wakati wa enzi ya ukoloni katika Afrika Mashariki, haja ya kuwepo kwa lugha moja itakayotumika hususani katika elimu katika nchi zote za makoloni ya Mwingereza wakati ule, yaani Tanganyika, Kenya, Uganda ilijitokeza. Matokeo ya haja hii ni kuchaguliwa kwa Kiswahili, hususani lahaja ya Kiunguja itumike kama lugha ya kufundishia mashuleni. Vilevile, matokeo ya haja hiyo yalikuwa ni kuundwa kwa Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki mnamo mwaka 1925 na kuanza kazi mwaka 1930 iliyopewa mamlaka ya kuisanifisha lugha ya Kiswahili, ili kuwe na namna moja rasmi ya kusema na kuandika katika Afrika Mashariki.

Baada ya nchi za Afrika Mashariki kupata Uhuru, haja ya kuwepo kwa lugha moja kwa kila nchi kwa ajili ya mawasiliano na wananchi, na katika shughuli mbalimbali za kiserikali na za kijamii ikajitokeza. Tanganyika ilipojipatia uhuru

mwaka 1961 (Tanzania tangu 1964) ikajichagulia Kiswahili kilichokuwa kimekwishaenea nchi nzima kiwe lugha ya Taifa na Kiingereza kiwe lugha rasmi katika masuala ya kiserikali na kimataifa. Kenya ilipopata uhuru mwaka 1963, kwa kuwa haikuwa na lugha iliyokuwa imeenea nchi nzima, na kwa kuhofia mivutano ya kuchagua lugha moja ya wenyeji, haikuteuwa lugha ya taifa. Hata hivyo, Kiingereza kiliteuliwa kiwe lugha rasmi katika masuala ya kitaifa na kimataifa. Kiswahili ambacho kilikwishaanza kuongelewa na watu wengi, kilitumika katika kuwasiliana na wananchi katika mikutano ya siasa, biashara n.k. Uganda ilipata uhuru mwaka 1962. Ijapokuwa katika kipindi hicho lugha ya Luganda ilikuwa imekwishaenezwa nchini na watawala wa Kiganda, si Luganda wala lugha nyingine yoyote ya wenyeji iliteuliwa kuwa lugha ya taifa. Whiteley (1969) anadai kuwa

> 'uteuzi wa watawala kutoka Buganda kutawala sehemu mbalimbali za Uganda, kulichangia kueneza lugha, lakini watawala hawa walionekana kama walikuwa wanapanua utawala wa Buganda, hivyo mwishowe lugha yao na wao wenyewe walichukiwa' (uk. 69).

Lugha nyingine ambayo ilikuwa imeenea kwa kiasi fulani nchini ilikuwa Kiswahili. Ijapokuwa pendekezo la Gavana Sir W.F. Gowers la kukifanya Kiswahili kiwe lugha ya elimu na utawala na vilevile kama lugha mawasiliano (lingua franca) nchini kote lilipingwa vibaya na Kabaka, Sir Daudi Chwa mwaka 1929, Kiswahili kiliendelea kupata mashiko. Whiteley (1969:70-71) anaripoti kuwa Kiswahili kiliendelea kutumiwa na polisi, sehemu za Kaskazini kuwasiliana na watu ambao hawajui Kiingereza na Luganda. Vilevile Wanilotiki wa Uganda walitumia sana Kiswahili kuwasiliana na makabila mengine. Kiswahili kilitumika pia kwenye mipira, na sehemu nyingine ambazo Kiingereza na Luganda havikuhitajika au havikuwezekana kutumika.

Hata hivyo, ili kukidhi haja ya mawasiliano, baada ya uhuru, Kiingereza kiliteuliwa kiwe lugha rasmi katika masuala ya kitaifa na kimataifa. Matumizi ya Kiswahili nchini Uganda yameshika kasi baada ya kuondolewa madarakani kwa Idd Amina Dada na kuingia madarakani kwa Rais Yoweri Muzeveni, ambaye aliishi Tanzania kwa miaka kadhaa na elimu yake ya Chuo Kikuu kuipatia huko.

Katika bara la Afrika kwa ujumla, uundwaji wa ushirikiano wa kiuchumi miongoni mwa nchi huru, pamoja na mambo mengine, ulizingatia kigezo cha lugha ya mawasiliano. Kihistoria, ushirikiano baina ya Waafrika ulianza kabla nchi za Afrika hazijapata uhuru kati ya mwaka 1920-1957 chini ya dhana ya Upanafrika. Lengo kuu lilikuwa kuzikomboa nchi hizo zitoke kwenye utawala wa kikoloni. Ushirikiano baina ya nchi huru za Kiafrika ulianza baada ya nchi za Afrika kuanza kupata uhuru kati ya mwaka 1957 na 1960. Malengo makuu ya awali ya ushirikiano yalikuwa kwanza, ni kupigania uhuru wa makoloni yaliyobaki na pili, kuunda muungano wa kisiasa wa bara zima chini ya serikali moja ya shirikisho. Baada ya nchi nyingi za Kiafrika kujipatia uhuru kuanzia mwaka 1960, mgawanyiko ukaanza kujitokeza na wazo la kuwa na muungano wa kisiasa likaanza kufifia. Badala ya kufikiria muungano wa nchi zote za

Afrika makundi mbalimbali yakaanza kujitokeza. Kwa mfano mwaka 1961, Ghana, Guinea, Misri, Mali, Morocco, Libya na Algeria wakaunda kundi la Casablanca, makoloni yaliobaki ya Wafaransa pamoja na Nigeria, Ethiopia, Liberia, na Sierra Leone wakaunda kundi la Monrovia. Mgawanyiko huu ulivunjwa makali yake baada ya Kwame Nkrumah, Sekou Toure na Modibo Keita wakiungwa mkono na Mfalme Haile Selassie kuitisha mkutano wa kilele wa Nchi huru za Kiafrika Mei 1963 na kuunda Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika (OAU) Mei 25, 1963. (Asante, 2002).

Baada ya kuanguka kwa wazo la kuwa na muungano wa kisiasa wa bara lote, wazo la kuwa na vyombo vya kujikomboa kutokana na utegemezi wa kiuchumi lilijitokeza. Wazo hili lilisababisha kuundwa kwa vyombo vya kiuchumi vya kikanda ambapo vikundi viliundwa kwa misingi ya lugha za mawasiliano. Kwa mfano, nchi zinazozungumza Kifaransa ziliunda Chama cha Forodha cha Nchi za Afrika Magharibi (UDEAO) mwezi Juni 1966, Jumuiya ya Uchumi ya Afrika Magharibi (CEAO) mwaka 1973, Chama cha Forodha na Uchumi cha Afrika ya Kati (UDEAC) mwaka 1966, Umoja wa Mto Senegal (OERS) ambao mwaka 1972 ukawa Umoja wa Kuendeleza mto Senegal (OMVS), na Ushirikiano wa Wanachama Tisa wa Kamati ya Kudumu ya Ushauri wa Maghreb mwezi Novemba 1965. Vyombo hivi vingi havikudumu na vile vilivyodumu havikuzaa matunda yaliyotarajiwa. (Asante, 2002).

Kwa upande wa nchi zinazozungumza Kiingereza, hapakuwepo na jumuiya za kiuchumi za kikanda zilizoundwa katika miaka ya mwanzo ya uhuru isipokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyoanzishwa na nchi za Tanzania, Kenya na Uganda mwezi Juni 1967. Muungano huu ambao uliendesha mambo mengi kikanda kama vile biashara ya nje, sera ya fedha, miundo-mbinu ya usafiri na mawasiliano, na elimu haukudumu na ulivunjika mwezi Julai 1977.

Wakati wa Shirikisho la Afrika Mashariki, lugha iliyokuwa inatumika wakati huo ilikuwa ni Kiingereza. Haja ya kuwepo kwa Kiswahili haikujitokeza sana kwa sababu ushirikiano huu ulikuwa unatekelezwa na asasi za juu husika za Kitaifa na zile za Afrika Mashariki zilizoundwa chini ya ushirikiano huu. Kwa mfano Bunge la Afrika Mashariki, Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki, Shirika la Reli la Afrika Mashariki, Shirika la Ndege la Afrika Mashariki, Makao Makuu ya Afrika Mashariki n.k. Haja ya kutumia Kiswahili haikujitokeza kwa vile, vyombo vilivyokuwa vinaendesha shirikisho hili vilikuwa vinaendeshwa na wasomi wanaoelewa Kiingereza. Maingiliano baina ya wananchi wa kawaida wakati huo yalikuwa ni madogo sana kutokana na uwezo na mwamko wa wananchi wa wakati huo.

Hata hivyo, hivi karibuni pamezuka ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda ambao unavuka mipaka ya lugha. Kwanza kuna Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS) ambayo imeanzishwa Mei, 1975. Jumuiya hii inajumuisha nchi tano zinazozungumza Kiingereza, nane Kifaransa, mbili Kireno na moja Kiarabu.

Pili, kuna Mkutano wa Kuratibu Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADCC sasa SADC) ulioanzishwa rasmi Aprili 1980 na kutiwa saini na nchi za mstari

wa mbele yaani Angola, Msumbiji, Tanzania na Zambia na baadaye Lesotho, Malawi, Swaziland na Zimbabwe.

Tatu, kuna Eneo la Upendeleo wa Biashara kwa Nchi za Afrika Mashariki na Kusini (PTA) lililoanzishwa na nchi nane Desemba 1981 na kuzinduliwa rasmi Julai 1984. Nne ni Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika ya Kati (ECCAS) ikijumuisha wanachama wa UDEAC na wale wa Jumuiya ya Uchumi ya Maziwa Makuu.

## 1. LUGHA-MAWASILIANO

Dhima kuu ya lugha yoyote ni kukidhi haja ya mawasiliano katika jamii yenye utamaduni mmoja. Pamoja na dhima hiyo muhimu, lugha hutumika pia kama kitambulisho cha jamii fulani na vilevile kama njia mojawapo ya kuelezea na kuhifadhia utamaduni wake.

Hata hivyo, kutokana na maingiliano ya watu, zipo lugha ambazo zimevuka mipaka ya jamii zao husika na kutumika kama vyombo vya mawasiliano katika jumuiya kubwa zaidi zenye watu wenye lugha na tamaduni tofauti. Lugha kama hizo hazikidhi haja ya mawasiliano ya jamii zao tu, bali hukidhi haja ya mawasiliano katika jamii pana zaidi katika nchi, kanda, au dunia nzima. Lugha zenye dhima kama hii, hujulikana kama lugha-mawasiliano (lingua franca). Katika Kamusi ya Isimu na Lugha ya TUKI (1979:12) lugha-mawasiliano imetafsiriwa kuwa ni lugha inayotumika kwa mawasiliano katika eneo lenye lugha nyingi tofauti (uk. 12).

Kwa mujibu wa Trudgill (1974), ‘nchi inaweza kuwa na lugha rasmi ya kutumia katika mawasiliano, lakini zikawepo lugha nyingine nchini ambazo hutumika katika viwango vya kifamilia, kikabila, kiwilaya au kimkoa’ (uk. 12). Kwa kuangalia Afrika Mashariki, lugha zinazoweza kutumika kiufanisi kuhudumia Afrika Mashariki nzima ni mbili tu. Lugha ya Kiingereza ambayo huweza kutumiwa baina ya serikali, wasomi na asasi za kikanda kama vile vyuo vikuu, mashirika ya kitaifa na kimataifa na mabunge. Kwa upande wa pili, lugha ya Kiswahili huweza kutumika katika nyanja ambamo Kiingereza huweza kutumika pamoja na maeneo ambamo Kiingereza hakiwezi kutumika, kama vile mawasiliano baina ya wananchi na wafanyabiashara wa kawaida katika nchi hizo. Ni katika kiwango hiki cha pili ambapo Kiswahili pekee hutamba. Kwa hiyo Kiswahili kina nafasi nzuri ya kushiriki katika ujenzi wa jamii mpya ya Afrika Mashariki.

Massamba (1990) anadai kuwa Kiswahili ni lugha-mawasiliano kwa vile ni ‘lugha isiyokuwa na mipaka ama ya kieneo au kitaifa’ (uk. 4). Kauli hii imetokana na ukweli kwamba Kiswahili ni chombo cha mawasiliano katika jamii kubwa zaidi nchini Tanzania na Kenya, na kimevuka mipaka na kuingia Uganda, Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo na kwingineko.

## 2. LUGHA KAMA KITAMBULISHO NA KIUNGANISHI CHA JAMII

Kutokana na ushirikiano ulioanzishwa wa nchi za Afrika Mashariki, suala la kuwa na kitu cha kuwatambulisha watu wa Afrika Mashariki pamoja na kuwa na mfumo wa kuwaunganisha watu hawa ili wajione ni kitu kimoja na wenye lengo moja kwa maslahi ya maendeleo yao ni muhimu sana.

Kuna mambo mengi ambayo watu wa Afrika mashariki wanaweza kuyatumia kama kitambulisho chao. Baadhi ya mambo hayo ni kama vile ushirikiano wenyewe ulioanzishwa wa kisiasa na kiuchumi, pamoja na mashirikiano mengine ya kijamii kama vile katika michezo, elimu n.k. Mambo mengine yanayoweza kutumika kuwatambulisha watu wa Afrika Mashariki yanaweza kuwa ya kijiografia. Kwa mfano watu wa Afrika Mashariki wanaweza kujinasibisha na mlima Kilimanjaro, maziwa makuu, chanzo cha mto Nili, aina za madini na mazao.

Hata hivyo, njia nyingine mwafaka ya kujitambulisha ni lugha. Mulokozi (2000) anadai kuwa 'lugha ni msingi wa utambulisho wa watu' (uk. 72). Mpaka sasa barani Afrika, utambulisho katika maeneo ya kikanda umekuwa ukifanywa kwa kutumia lugha za kigeni. Kwa msingi huo utasikia kuna ushirikiano wa nchi zinazozungumza ama Kiingereza au Kifaransa. Itakuwa jambo jema kama katika karne tuliyonayo, nchi za Afrika zitajitambulisha kwa lugha zao za Kiafrika. Mfano kundi la nchi zinazozungumza Kihausa au Kizulu au Kiswahili, n.k.

Kwa upande wa nchi za Afrika Mashariki na Kati, yaani Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, lugha inayoweza kuchaguliwa kama lugha ya kuzitambulisha na kuziunganisha jamii katika nchi hizi ni Kiswahili. Kiswahili kimevuka mipaka ya nchi zao asilia yaani Tanzania na Kenya na kuenea karibu kwenye nchi zote Afrika Mashariki na Kati japo kwa viwango tofauti. Hakuna lugha nyingine ya Kiafrika katika nchi hizi za Afrika Mashariki yenye sifa kama hiyo. Kwa hiyo, Kiswahili kinafaa kuchukuliwa kama lugha ya utambulisho wa wananchi wa Afrika Mashariki na vilevile lugha ya kuwaunganisha.

Mulokozi (2000:75) amezigawa nchi za Kiafrika katika makundi 4:

1. Nchi zenye lugha moja;
2. Nchi zenye lugha mbili au zaidi lakini zenye lugha kuu kadhaa za kikanda/lugha mawasiliano (lingua franca);
3. Nchi zenye lugha nyingi lakini zenye lugha-mawasiliano moja au mbili za wenyeji;
4. Nchi zenye lugha nyingi ambazo hazina lugha-mawasiliano au lugha ya kikanda inayozungumzwa na watu wengi.

Mulokozi (2000) anadai kuwa nchi zinazoingia kwenye kundi la tatu ni kama vile Tanzania na Kenya ambazo zina lugha nyingi lakini zina Kiswahili kama lugha ya watu wengi. Vilevile, Uganda yenye lugha nyingi lakini ina Luganda na Kiswahili kama lugha zinazozungumzwa na wengi. Mulokozi (2000)

anapendekeza kuwa katika kundi hili la tatu, nchi hizo zinatakiwa kuchukua lugha-mawasiliano moja ya wenyeji iwe lugha rasmi na lugha ya taifa.

Tukiangalia nchi za Afrika Mashariki kwa pamoja, tunaona kuwa hakuna lugha-mawasiliano nyingine katika kanda hii inayoweza kuchukua dhima inayotajwa na Mulokozi (2000) isipokuwa Kiswahili. Kiswahili pekee ndicho kinachoweza kuchukuliwa kama lugha ya kuwaunganisha na kuwatambulisha watu wa Afrika Mashariki popote duniani.

## 3. Matumizi ya Kiswahili katika Afrika Mashariki

Katika nchi za Afrika Mashariki, lugha za Kiingereza na Kiswahili zinatumika sana katika mawasiliano. Nchini Tanzania, Kiswahili hutumika kama lugha ya Taifa, lugha rasmi katika shughuli za serikali na bunge, lugha ya mawasiliano katika shughuli za biashara za nchini, na baina yake na nchi jirani, lugha inayotumika katika vyombo vya habari na vilevile lugha ya kufundishia katika shule za msingi. Nchini Kenya, Kiswahili hutumika kama chombo cha mawasiliano baina ya watu wa makabila mbalimbali, katika mikutano ya kisiasa na wananchi, katika shughuli za biashara za nchini na baina yake na nchi jirani, na hufundishwa kama somo katika shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu. Nchini Uganda, Kiswahili hutumiwa zaidi na askari na katika kufanya mawasiliano na wageni kutoka nchi jirani za Afrika Mashariki hususani katika biashara, shughuli za kijamii n.k. (Whiteley, 1969). Vilevile Kiswahili sasa hufundishwa kama somo katika shule za msingi na sekondari. (Masau, 2000). Mwansoko, (2002) alipokuwa anahudhuria Kongamano la Kikanda la Maziwa Makuu, mjini Kampala Uganda, mwezi Aprili 2002, ameshuhudia kuwa 'mjini Kampala, watu wengi huzungumza Kiswahili hususani madukani, vilabuni, sokoni, mpirani na madereva wa taksi. Hata hivyo amebaini kuwa wasomi kwa kiasi fulani wanakikwepa'. Pamoja na hayo, Chuo Kikuu cha Makerere kina Idara ya Kiswahili ambayo hufundisha isimu na fasihi katika Kiswahili.

Pamoja na kutofautiana katika viwango vya matumizi ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki, bado linapokuja suala la mawasiliano katika ngazi zote kwa watu wote wa Afrika Mashariki, Kiswahili hupewa nafasi kubwa ukilinganisha na nafasi inayopewa Kiingereza. Kwa mfano, wakati nchini Tanzania Kiswahili hutumiwa na watu kiasi cha asilimia 100%, Kiingereza hutumiwa na watu kiasi cha asilimia 10%. Kwa upande wa Kenya, wakati Kiswahili huweza kutumiwa na watu zaidi ya asilimia 80%, Kiingereza huweza kutumiwa na watu kiasi cha watu asilimia 20% tu. Nchini Uganda wakati Kiswahili huweza kutumiwa na watu kiasi cha asilimia 50%, Kiingereza hawazidi asilimia 20%. Kwa takwimu hizi, inaonekana kuwa Kiswahili kina nafasi kubwa ya kuchangia katika kujenga ushirikiano mpya wa watu wa Afrika Mashariki kuliko Kiingereza. Kwa hiyo, ipo haja ya kuwa na mikakati madhubuti ya kukiendeleza Kiswahili katika Afrika Mashariki.

## 4. UUNDAJI WA USHIRIKIANO MPYA WA AFRIKA MASHARIKI

Katika miaka ya hivi karibuni, hususani baada ya kuanzishwa kwa sera za masoko huria, hali ya Afrika Mashariki imebadilika sana. Hii inatokana na mwamko uliojitokeza miongoni mwa wananchi wa kawaida kujitokeza katika kufanya shughuli nyingi za biashara ambazo zamani zilikuwa zinafanywa na serikali au makampuni ya kitaifa au ya kigeni. Kwa sasa, mchango wa watu wa kawaida katika kuwafikia na kuwaunganisha watu wa Afrika Mashariki ni mkubwa mno ukilinganisha na ule wa serikali na makampuni ya kitaifa au ya kigeni. Wananchi wa kawaida ambao ni wafanyabiashara ndiyo kiungo kikubwa kwa sasa baina ya wazalishaji na wananchi. Maingiliano haya ambayo yatashika kasi jinsi ushirikiano mpya wa Afrika Mashariki utakavyokuwa unaendelea kukua na kutekelezwa, yataanza kuibua suala la lugha ya kutumika katika kuwaunganisha na kuwashirikisha watu wengi zaidi na wa viwango tofauti vya elimu.

Tarehe 30.11.2001, serikali za Tanzania, Kenya na Uganda, zilitiliana saini mkataba wa ushirikiano mpya wa Afrika Mashariki. Ushirikiano huu mpya umeanzishwa kwa tahadhari kubwa ili usikumbwe na matatizo yaliotokea kwenye ushirikiano wa awali, matatizo yaliyosababisha kuvunjika kwa ushirikiano huo. Ushirikiano mpya wa Afrika Mashariki umefungua milango mingi ya ushirikiano katika nyanja za biashara, elimu, uchumi, kijamii na kisiasa. Iko azma ya kuwa na mipaka huru baina ya nchi husika, soko la pamoja la bidhaa za biashara baina ya nchi hizo, sarafu moja n.k.

Mazingira kama hayo yatafanya maingiliano baina ya watu wa Afrika Mashariki kuwa makubwa zaidi hususani kwenye nyanja za kiuchumi, kielimu na kijamii. Mazingira kama hayo yatanufaika zaidi kama Kiswahili kitatiliwa maanani katika nchi hizi. Hapa hatuna maana ya kusema kuwa Kiingereza hakithaminiwi, bali tunachodai ni kuwa serikali zetu tatu zinatakiwa kuwekeza zaidi katika kupanua uelewa na matumizi ya Kiswahili katika kanda hii.

Mwezi Aprili, 2002, mjini Kampala Uganda kuanzia tarehe 8-11, kulifanyika Kongamano la Kikanda la Nchi za Maziwa Makuu. Kongamano hilo ambalo liliandaliwa na Mfuko wa Mwalimu Nyerere, lilihusu '*Uimarishaji wa Mashirikiano ya Kikanda na Kuweka Agenda ya Milenia ya Utamaduni wa Amani, Umoja na Maendeleo ya Watu*'. Katika Kongamano hilo, pamoja na mambo mengine, suala la lugha lilipewa nafasi ya kuzungumzwa. Majadiliano kuhusu vyombo vya habari na maendeleo ya Kiswahili yalibainisha mambo yafuatayo:

- Ukanda wa Maziwa Makuu unahitaji lugha ya kuwatambulisha na kuwaunganisha. Lugha ambayo kwa sasa imeenea katika nchi zote za kanda hii ni Kiswahili. Kwa hiyo Kiswahili kinaweza kuzileta pamoja nchi zote katika kanda.
- Kuendelea kutumia lugha za Ulaya kama vile Kiingereza na Kifaransa kumechangia sana kukwamisha mawasiliano katika kiwango cha kitaifa

na kikanda. Kiswahili kinaweza kutoa nafasi ya mawasiliano kati ya serikali na watu wake.

- Kiswahili kimekwishaonekana kama lugha-mawasiliano iliyo bora na sio tu katika kanda ya Maziwa Makuu, bali pia katika Afrika. Tangu mwaka 1955 majadiliano katika vikao mbalimbali yameonyesha matumizi ya Kiswahili kama lugha ya Upanafrika.
- Hadhi ya Kiswahili katika Ukanda wa Maziwa Makuu hukifanya kiwe lugha pekee inayofaa kuendeleza kuwa lugha-mawasiliano ya kikanda. Ni lugha ya taifa katika nchi tatu katika kanda, inafundishwa mashuleni karibuni katika nchi zote, na lugha ya mawasiliano miongoni mwa jamii za lugha mbalimbali za wenyeji. Kwa ujumla inakadiriwa kuwa Kiswahili kinazungumzwa na watu kadri ya milioni 80 katika Ukanda wa Maziwa Makuu (uk. 3-4).

Maazimio ya Kongamano kuhusu lugha ambayo yalisomwa mbele ya Wakuu wa Nchi za Maziwa Makuu, yaani Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi, kabla hawajaanza mkutano wao wa kilele, yalisema kuwa ‘Kiswahili kinaweza kuchukua dhima ya kuwaunganisha watu katika kiwango cha kikanda. Hivyo, Kiswahili kipewe hadhi ya kuwa lugha-mawasiliano (lingua franca) ya kikanda. Lugha nyingine zitakuwa na dhima zao katika kiwango cha kieneo, kitaifa au kimataifa’ (uk. 5).

## 5. Mikakati ya Kutumia Kiswahili kama Lugha-mawasiliano Katika Afrika Mashariki

Katika kufikiria kwa dhati dhima ya Kiswahili kama chombo cha mawasiliano, utambulisho na kiunganishi cha watu wa Afrika mashariki, kuna haja ya kuwa na mikakati bayana ya kufikia lengo hilo. Hapa chini panatolewa mapendekezo machache ambayo yanaweza kuchukuliwa kama sehemu ya mkakati.

### 5.1 Dira ya Kimkakati

Ili kufanikisha lengo letu, kutakuwa na haja ya kuwa na dira ya kimkakati. Dira itatuelekeza kile kinachotakiwa kufikiwa na kutekelezwa. Dira hiyo ya kimkakati ambayo itakuwa ndani ya sera ya lugha ya Afrika Mashariki, itayarishwe na chombo husika cha Ushirikiano wa Afrika Mashariki na kupitishwa na Bunge lake husika ili kuwa sheria. Kwa kuwa Kiswahili kwa sasa ndiyo lugha pekee inayotumiwa na wananchi wengi katika Afrika Mashariki na kwa kuwa baadhi ya vyombo vya kikanda vimeanza kukipendekeza kuwa lugha-mawasiliano ya Afrika Mashariki, basi sera yetu ya lugha itakapokuwa imepitishwa, inapendekezwa kuwa dira yetu ya kimkakati ihusishe kukipa uwezo Kiswahili ili kiweze kumudu na kutumika katika nyanja zote za

mawasiliano, na vilevile kukuza uwezo wa wananchi wake katika kukielewa na kukizungumza Kiswahili.

## 5.2 MALENGO YA KIMKAKATI

Dira ya kimkakati itatuelekeza kwenye kuunda na kuendeleza asasa za Kiswahili katika Afrika Mashariki, na kutilia mkazo mafunzo ya Kiswahili kwa watu wake. Katika kufanikisha hilo, malengo ya kimkakati yawe ni pamoja na uundaji na ukuzaji wa asasi za kukuza na kusimamia maendeleo ya Kiswahili, kuhimiza na kusimamia matumizi ya Kiswahili katika vyombo vyake kama vile redio, magazeti, mabunge n.k., na kuhimiza mafunzo ya Kiswahili katika nchi husika kwa kubadilishana walimu, vitabu na uzoefu. Malengo hayo ya kimkakati yanaweza kutekelezwa kwa kuanzisha mambo yafuatayo.

### 5.2.1 Baraza la Kiswahili la Afrika Mashariki

Ili kutimiza lengo la kuwa na asasi za kikanda za kukikuza na kukieneza Kiswahili, kutakuwa na haja ya kuwa na Baraza la Kiswahili la Afrika Mashariki. Baraza hili litakuwa chombo muhimu sana katika kukiendeleza Kiswahili katika kanda hii na linatakiwa lisiwe chombo cha kitaaluma kwa asilimia 100%, bali kiwe pia chombo cha kisiasa na kisera. Pendekezo kama hili lilikwishawahi kupendekezwa katika mkutano wa Washikadau wa Utamaduni, Michezo, Sanaa na Uridhi, uliofanyika Arusha mwaka 2001 (Kishe, 2002:16)

Kama ilivyokuwa kwa Kamati ya Lugha ya Afrika mashariki, Baraza litatakiwa kutoa ithibati kwa kazi mbalimbali za maandishi na kusimamia usanifishaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa kuwa kitaifa kutakuwa na asasi zinazoendeleza Kiswahili, chombo cha kikanda kitatoa maelekezo katika vyombo na asasi za kitaifa ili kupata usawazisho wa kikanda. Sera ya lugha itahitajika sana kwa kuwa ndiyo itakayoonyesha mipaka ya lugha ya Kiswahili kama lugha-mawasiliano, lugha za wenyeji, na lugha za kigeni kama vile Kiingereza na Kifaransa.

Baraza litatakiwa kuwa chombo cha uhamasishaji wa matumizi ya Kiswahili Afrika Mashariki. Mbinu mbalimbali zinatakiwa kubuniwa. Baadhi ya mbinu hizo ni pamoja na kuwa na mashindano ya wanafunzi, waandishi na wasanii mbalimbali. Vilevile Baraza litatakiwa kufanya kazi ya kuzihamasisha serikali zetu tatu ziweze kukipa nafasi ya kutosha ya kutumika katika nyanja, vyombo na asasi mbalimbali ili kiweze kukua na kuenea katika kila kona.

### 5.2.2 Taasisi ya Utafiti wa Lugha ya Kiswahili ya Afrika Mashariki

Katika kutekeleza lengo la kuwa na asasi za kuendeleza Kiswahili, kutakuwa na haja ya kuwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili ya Kikanda. Tofauti na Baraza la Kiswahili la Afrika Mashariki, taasisi hii itakuwa ya kitaaluma na pamoja na mambo mengine inaweza kushughulikia miradi ya uendelezaji wa Kiswahili ya kikanda. Inaweza pia kuratibu semina, makongamano na mafunzo ya kikanda. Kwa mfano, mradi wa kamusi mama ya Kiswahili ambayo itaonyesha Kiswahili kama kinavyozungumzwa katika nchi mbalimbali za Afrika mashariki unaweza kusimamiwa na taasisi hii.

### 5.2.3 Matumizi ya Kiswahili katika Bunge la Afrika Mashariki

Katika kukifanya Kiswahili kitumike katika nyanja zote na katika vyombo na asasi mbalimbali katika Afrika mashariki, mfano mzuri utakuwa ule wa kukitumia katika Bunge letu la Afrika Mashariki. Uamuzi huo sio kwamba utatoa changamoto kwa asasi nyingine, bali utatoa ushawishi mkubwa kwa watu wa Afrika Mashariki kukienzi na kukiendeleza na kukitumia Kiswahili katika maeneo yao.

### 5.2.4 Kiswahili kifundishwe mashuleni

Katika kutimiza lengo la kutoa mafunzo ya Kiswahili kwa watu wa Afrika Mashariki, ili kuongeza uwezo wao wa kusikia na kukizungumza Kiswahili, kutakuwa na haja ya kukifundisha mashuleni. Katika nchi kama Tanzania na Kenya, Kiswahili kinaweza kuwa lugha ya kufundishia katika shule za msingi na kama somo katika shule za sekondari. Katika nchi kama vile Uganda, Rwanda na Burundi, kwa kuanzia, Kiswahili kinaweza kufundishwa kama somo katika ngazi zote za elimu.

Utekelezaji wa suala hili utaibua suala la vitabu na walimu. Nchi za Afrika Mashariki zinaweza kushirikiana katika jambo hilo, kwa kubadilishana vitabu, kubadilishana uzoefu katika semina mbalimbali na mafunzo na kuazimana walimu katika ngazi zote. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili ya Afrika Mashariki ikishirikiana na wizara husika inaweza kuratibu suala hili.

### 5.2.5 Matumizi ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari

Katika kutekeleza lengo la kukifikisha Kiswahili katika kila kona, kutakuwa na haja ya kuhimiza vyombo vyetu vya habari kukipa nafasi Kiswahili katika magazeti, redio na televisheni. Faida kubwa inayoweza kupatikana kutokana na mpango huu ni kwamba vyombo vya habari vitasaidia kukisambaza Kiswahili kwa haraka na kukuza uwezo wa lugha wa watumiaji wake. Faida ya pili, ni

kwamba vyombo vya habari vitasaidia katika kufikisha habari kwa watu wengi ambao kwa namna moja au nyingine hawajui Kiingereza.

### 5.2.6 Utungaji wa Kamusi za Kiswahili

Utungaji wa Kamusi za Kiswahili za lugha moja au lugha mbili, utabidi utiliwe maanani sana. Pamoja na ukweli kuwa kamusi huhifadhi lugha katika maandishi kwa ajili ya vizazi vijavyo, kamusi zinasaidia sana watu katika kujifunza lugha.

Kwa kuwa ukiangalia Afrika ya Mashariki kwa ujumla utagundua kuwa bado kuna sehemu nyingi zinatakiwa kuimarishwa mintarafu kiwango chao cha Kiswahili, basi utunzi wa kamusi hautaepukika. Ili kusaidia uelewa, kuna haja ya kutunga kamusi za lugha moja na kamusi za lugha mbili hususani Kiswahili na lugha za wenyeji. Kazi za utungaji wa kamusi zinaweza kufanywa na wataalamu wa lugha au asasi za lugha kama vile taasisi za uchunguzi wa Kiswahili za taifa na kikanda pamoja na mabaraza ya Kiswahili ya taifa na kikanda, na watu binafsi.

## 6. HITIMISHO

Tumesema kwamba lugha ni chombo muhimu sana cha mawasiliano na kwamba maingiliano ya watu wenye utamaduni tofauti na kuzungumza lugha tofauti mara nyingi huzusha haja ya kutumia lugha moja itakayounganisha makundi yote ya lugha husika.

Pia tumesema kuwa lugha ni chombo muhimu sana katika kuwaleta watu pamoja. Watu hutumia lugha katika kujitambulisha na kuonyesha ukaribu na udugu na mshikamano wao. Kwa hiyo, lugha ni chombo muhimu cha kuleta mshikamano miongoni mwa watu.

Dhana ya kuwa na lugha moja miongoni mwa jamii zinazozungumza lugha mbalimbali ni kongwe sana na imejitokeza tangu watu wa jamii mbalimbali walipoanza kuingiliana kwa ajili ya biashara na masuala mengine ya kijamii. Barani Afrika haja hiyo ilijitokeza kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya uhuru.

Kutokana na haja hiyo, matumizi ya baadhi ya lugha katika Afrika yamevuka mipaka ya jamii zao husika na kuingia hadi kwenye jamii nyingine katika ngazi ya eneo, wilaya, mkoa, nchi, na kanda. Mpaka sasa hatuna lugha katika Afrika ambayo inatumika katika bara zima, lakini lugha za kikanda tunazo. Lugha zilizojipatia sifa hiyo ya kuvuka mipaka ya jamii zao hujulikana kama lugha-mawasiliano (lingua franca). Katika Afrika Mashariki lugha iliyojitokeza kuwa na sifa hiyo ni lugha ya Kiswahili. Lugha hii kwa sasa imevuka mipaka ya jamii yake ya Waswahili na kutumiwa na watu wote wa Tanzania, asilimia kubwa ya watu wa Kenya na vilevile katika kiwango cha kuridhisha nchini Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo.

Makala hii imebaini kuwepo kwa ushirikiano mpya wa mambo ya kibiashara na ya kijamii katika Afrika Mashariki hususani Tanzania, Kenya na Uganda. Imebainika kuwa ushirikiano kama huu ambao utawashirikisha wananchi wengi wa nchi hizi katika viwango vyote mpaka vijijini, utachochea haja ya kuwepo kwa lugha moja ya mawasiliano ambayo itawaunganisha na kuwatambulisha. Makala hii imebaini kuwa lugha yenye sifa kama hiyo ni Kiswahili. Lugha ya Kiswahili imevuka mipaka ya kieneo na kitaifa. Kwa sasa ina sifa ya kuwa lugha ya kikanda. Lugha kama hii ambayo imepewa nafasi tangu enzi za ukoloni kukua na kuendelezwa, inafaa sana kuchukua dhima hiyo katika ukanda huu wa Afrika Mashariki.

Makala imebaini pia kuwa fikra na raghba za kuwa na lugha-mawasiliano katika Afrika Mashariki zimeelezwa pia na mikusanyiko mbalimbali iliyowaleta pamoja wananchi wa Afrika Mashariki. Kwa mfano, Mkutano wa Washikadau wa Utamaduni, Michezo, Sanaa na Urithi, uliofanyika Arusha mwaka 2001, ulibaini haja ya kuwa na Kiswahili kama lugha ya Afrika Mashariki na kupendekeza kuundwa kwa Baraza la Kiswahili la Afrika Mashariki litakalosimamia maendeleo ya Kiswahili. Vilevile Kongamano la Maziwa Makuu juu ya '*Uimarishaji wa Mashirikiano ya Kikanda na Kuweka Agenda ya Milenia ya Utamaduni na Amani, Umoja na Maendeleo ya Watu*' liliazimia kuwa Kiswahili kichukue dhima ya kuwaunganisha watu katika kiwango cha kanda. Hivyo Kiswahili kipewe hadhi ya kuwa lugha-mawasiliano ya kikanda.

Mwisho makala hii imependekeza kuwa ili hoja ya kuteua Kiswahili kama lugha ya Afrika Mashariki ifanikiwe, mambo kadhaa lazima yatekelezwe. Kwanza, pamoja na mambo mengine inapendekezwa kuwa kuwe na dira ya kimkakati ambayo italenga kwenye kukipa uwezo Kiswahili ili kiweze kumudu na kutumika katika nyanja zote za mawasiliano. Vilevile kukuza uwezo wa wananchi wake katika kukielewa na kukizungumza Kiswahili. Pili, inapendekezwa kuwe na malengo ya kimkakati ambayo yatasaidia katika kufikia dira ya kimkakati. Katika malengo ya kimkakati inapendekezwa kuwe na (a) Baraza la Kiswahili la Afrika Mashariki, (b) Taasisi ya Utafiti wa Lugha ya Kiswahili ya Afrika mashariki, (c) Matumizi ya Kiswahili katika Bunge la Afrika Mashariki, (c) Ufundishaji wa Kiswahili Mashuleni, (d) Matumizi ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari, na mwisho (e) Utungaji wa Kamusi za Kiswahili.

## MAREJEO

Asante, S.K.B na Chanaiwa, D. 1999.
Upana-Afrika na Ushirikiano wa Kikanda. Katika Mazrui Ali A. na C. Wondji (Wahariri) (1999), *Historia Kuu ya Afrika: Juzuu lililofupishwa*, TUKI/UNESCO: Dar-es-Salaam.

Kishe, A. 2002.
*Kiswahili As a Vehicle of Unity and Development in the Great Lakes Region*. A paper presented at the Regional Conference on the Great Lakes Region on the Agenda for the Millennium, Kampala, Uganda, 8-11, Aprili, 2002.

Massamba, D.P.B. 1990.
*Kiswahili kama Lugha ya Mawasiliano na matumizi yake katika Vyombo vya Habari*. Makala iliyotolewa kwenye Semina ya Kanda kuhusu Sera na Mipango ya Kushirikisha Vyombo vya Habari katika Kukuza na Kueneza Kiswahili katika Nchi Zinazotumia Kiswahili.

Mulokozi, M.M. 2000.
*Language, Literature, and the Forging of a Pan-African Identity*, katika **Kiswahili Journal**, No. 63, uk. 71-80.

Mwansoko, H.J.M. 2002.
*Swahili Standardization as Vital Factor in Consolidating the Great Lakes Region Unity*. A paper presented at the Regional Conference on the Great Lakes Region on the Agenda for the Millenium, Kampala, Uganda, 8-11, April, 2002.

Nyerere Foundation, 2002.
Brief for the Leaders of the Region from the Symposium, Symposium on the Great Lakes Region.

Nyerere Foundation, 2002.
Review Report on the Media and Kiswahili Package, Symposium on the Great Lakes Region.

Whiteley, W. 1969.
*Swahili: The Rise of a National language.* Methuen & Co. LTD: London.